

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SIMU:025 - 2502260

Fax: 025 - 2500128



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 599
MBEYA.

Barua pepe: ded@mbeyadc.go.tz

Tovuti: Mbeyadc.go.tz.

09 NOVEMBA, 2018

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ONGEZEKO LA MAKUSANYO YA NDANI KWA MWEZI OKTOBA, 2018.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imekusanya shilingi milioni 457 kama mapato yake ya ndani kwa mwezi Oktoba, 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 ya pato la awali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Ndugu Stephen E. Katemba amesema kuwa ongezeko hilo limetoka na mikakati thabiti iliyowekwa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila mtumishi anashiriki katika zoezi la kukusanya mapato.

Katema amesema kuwa utaratibu wa kufuata fedha zilizo kusanywa kwa wakusanya mapato mara mbili kwa wiki, kufanya doria za usiku na mchana kwa watorosha mapato na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi umesaidia pia kuongeza pato la halmashauri.

Ameongeza kuwa Mpango wa halmashauri ni kuhakikisha inakusanya zaidi ya kiasi cha shilingi milioni 200 kwa kila mwezi kitakacho saidia kukamilisha miradi ya maendeleo iliyopitishwa kwenye bajeti ya 2018/2019.

Aidha Halmashauri inawaomba wananchi kuhakikisha wanatoa taarifa ya watorosha mapato pamoja na kuhakikisha wanakata vibali vya ujenzi pale wanapokuwa na mpango wa kujenga au kuendeleza ujenzi.

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari na uhusiano
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya
S. L P 599
Mbeya.